MARAFIKI WA HAKIKAZI

JARIDA MEI 2005

# HAKIKAZI CATALYST

Maarifa
Vitendo
Mabadiliko

## KARIBUNI

*Karibu kwenye toleo la kwanza la jarida la Hakikazi Catalyst. Jarida hili ni badala ya jarida la awali la kupashana habari. Kila miezi mitatu tutawajulisha, marafiki na wadau wetu, habari mpya za kuhusu shughuli na mipango ya asasi yetu wakati ikielekea katika kuadhimisha miaka mitano. Tunatumaini utalifurahia. Tungependa kujua mawazo yako*

*Ndani ya toleo hili:*

- Mafanikio ya SACCOS Terrat
- Orodha ya miongozo ya lugha rahisi inakua
- Maoni ya Mkurugrnzi
- Karangai – imejijengea jina
- Wafugaji na ushirikishwaji

## TERRAT WAANZISHA CHAMA CHA AKIBA NA MIKOPO - SACCOS

WAKAZI wa vijiji vya Mkonoo na Nodosoito, katika kata ya Terrat, Manispaa ya Arusha, wamepiga hatua kubwa ya kujikwamua kutoka kwenye umaskini, kwa kuanzisha chama chao cha akiba na mikopo (SACCOS). Mafanikio haya ni miongoni mwa maendeleo mengi yaliyofikiwa katika eneo hilo, tangu asasi ya Hakikazi ianze kujenga uwezo wa jamii miaka mitatu iliyopita. Kuendeleza mafanikio haya, Hakikazi ilichangia kiasi cha fedha kinachofanana kwa ushirika huo mpya ulioanzishwa ili kuhakikisha unakuwa imara kifedha kwa miaka ya mwanzo ya kuanza kufanya kazi.

Upatikanaji wa mikopo ni kikwazo kikubwa kinachowakabili wazalishaji na wafanyabiashara wadogo katika maeneo ambayo Hakikazi inafanya kazi, na wazalishaji wadogo wengi hushindwa kuweka akiba ya fedha ya kutosha kuanzia msimu wa kuvuna hadi kupanda ili kununulia pembejeo ikiwemo mbegu na mbolea.
Katika hali hii, kuwepo kwa mikopo kunaweza kuleta tofauti baina ya kuongezeka au kupungua kwa makundi yaliyo hatarini kuathirika na umasikini. Kadhalika wafanyabiashara wadogo na wajasiriamali chipukizi wanakabiliwa na ugumu wa kupata mitaji ya kuendesha biashara zao.

Hakikazi inafanya kazi na wanavijiji wa Mkonoo, Nadosoito na jamii nyinginezo 13, kubaini fursa za hali ya maisha endelevu ndani ya mazingira yao yenye vikwazo vya asili na kiuchumi. Sehemu kubwa muhimu ya kazi hii inahusisha uanzishwaji wa vikundi vya kuzalisha mali ambavyo vitatumia raslimali na maarifa kwa faida ya wanachama wao.
Pindi vitakapoanzishwa, vikundi vya kuzalisha mali vinayo nafasi nzuri ya kupiga hatua ya kupata vyanzo vya pesa na huduma ya ushauri kutoka kwa asasi binafsi na zile za umma.



*Vikundi vya Uzalishaji Mali - Nadosoito*

Kikundi cha kilimo cha Mkonoo kilihimizwa kutafuta huduma ya ugani kutoka Manispaa kuhusu mbinu na faida ya kulima mahindi yanayostahmili mvua chache. Matokeo ni kuzalisha mazao ya kuridhisha ingawa wanakikundi waliyaotesha wakati wa msimu uliokuwa na kiwango kidogo cha mvua.

Vikundi vingine hapa kijijini, vinajihusisha na uzalishaji wa maziwa, ufugaji wa mbuzi wa maziwa na upandaji wa miti kwa ajili ya kuhifadhi udongo.



# WAFUGAJI NA MCHAKATO WA SIASA

Hakikazi inashirikiana na asasi za kiraia za jamii ya wafugaji kuendesha uchambuzi shirikishi juu ya uwezo wao wa kitaasisi na utawala.

Kikundi cha mafunzo kutoka taasisi za wafugaji kinapatiwa msaada kuboresha ujuzi wa ushawishi wa sera kwa wafugaji katika ngazi zote za kijiji hadi taifa. Kama sehemu ya awamu ya kwanza ya mradi, Hakikazi inatoa majarida matatu ya lugha rahisi yanayoelezea sera muhimu na michakato ya kisiasa ya serikali ya Tanzania. Majarida yatachapishwa katika lugha za Kiingereza na Kiswahili na yanaitwa:

- Ufugaji ndani ya mfumo wa sera za Tanzania
- Ufugaji na Mkakati wa Taifa wa Kukuza na Kupunguza Umasikini
- Ufugaji na programu ya maboresho ya serikali za mitaa

Majarida hayo yatatumika kama zana za kuwezesha na kufundishia ili kuboresha uwezo wa vikundi vya jamii kuelewa mambo muhimu ya sera nchini Tanzania, umuhimu wake katika maisha endelevu ya wafugaji na jinsi ya kujihusisha kikamilifu katika michakato hii. Shughuli hizi ni sehemu ya awamu ya kwanza ya programu ya miaka 15 – 20 ambayo inalenga kuimarisha vyama vya kiraia vya wafugaji Afrika Mashariki nzima.

Taasisi ya RECONCILE na Taasisi ya kimataifa ya IIED zinatekeleza programu hii kwa msaada wa DFID, na shirika la maendeleo na ushirikiano la Uswiss na DANIDA.

Hakikazi imepata uzoefu mwingi wa kufanyakazi na wafugaji katika maeneo yake ya kazi ya kaskazini mwa Tanzania, ambako hulenga migogoro juu ya matumizi ya mali asili. Migongano ya kisheria kuhusu usimamizi wa ardhi, umeipa serikali kuu uwezo wa kuamua masuala ya matumizi ya ardhi bila kuwashirikisha wananchi katika baadhi ya maeneo.

Jumuia chache za wafugaji wasiohama na mifugo wameweza kufikia makubaliano ya manufaa na wawekezaji wa sekta ya utalii. Baadhi wamegundua kwamba haki yao ya matumizi ya ardhi ya asili imechukuliwa na serikali kuu na kupewa wawindaji au wachimbaji madini pasipo kuinufaisha jamii ya wafugaji.

Utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa unaweza kutoa fursa ya kuhakikisha kwamba sheria zinafafanuliwa na kwamba masuala ya usimamizi wa maliasili yanaamuliwa katika utaratibu shirikishi wa ngazi ya chini.

Changamoto kubwa mojawapo ya kukabiliana nayo itakuwa ni ufafanuzi mpya wa kisheria wa usemi wa "Ardhi isiyotumika". Kwa wakati huu, serikali kuu inaendesha sera za kukuza utumiaji wa ardhi ya aina hiyo kwa madhumuni ya uwekezaji.
Mara nyingi ardhi hizi zilikuwa zikitumika katika utaratibu endelevu kwa karne nyingi kama malisho ya msimu. Ni hivi karibuni tu kwamba shinikizo limetokea la kuwaondoa wafugaji kutoka maeneo ya hifadhi za taifa limesababisha matumizi zaidi ya ardhi ya uwindaji. Sera za kukuza maendeleo ya sekta ya mifugo inayolenga kutengeneza ranchi haitazuia kasi ya kuongezeka kushuka hadhi ya mzingira. ufugaji endelevu na utaratibu wa kuzalisha mifugo kwa ufanisi ndani ya soko la ndani na lile la kimataifa, unaweza kuleta faida endelevu zaidi kwa sekta zote za mifugo na jamii za wafugaji.

Kubakia pembezoni kwa jamii za wafugaji hakufungamani na suala la ardhi. Vipengele vingine vinajumuisha utoaji hafifu wa elimu na huduma za afya. Hakikazi inakusudia kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba wafugaji wanajenga uwezo wao wa kutetea kwa ufanisi haki zao za kujiendeleza.




Miongozo ya lugha rahisi ya Hakikazi Catalyist inapatikana kwenye tovuti yetu:- www.hakikazi.org

Au kwenye ofisi zetu:-

Hakikazi Catalyist,
Jengo la Meru Plaza
Barabara ya Esso
S.L.P 781
Arusha
Tanzania.

Simu: + 255 27 2509860

# KARANGAI - KITUO CHENYE MVUTO

Kijiji cha Karangai kilichopo Wilayani Arumeru, hivi karibuni kilitembelewa na Televisheni ya Taifa, ili kujulisha umma kuhusu mafanikio ya kuboresha hali ya maisha kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Ujumbe kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pia ulitembelea kijiji hicho kubaini hali halisi, ulifuatana na ujumbe wa ITV. Karangai ilichaguliwa kutembelewa na ujumbe huo, na Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kama mfano mzuri wa uhamasishaji wa jamii na maendeleo.

Hakikazi imekuwa ikishirikiana na kijiji cha Karangai kwa miaka mitatu na nusu sasa. Ushirikishwaji umezingatia falsafa ya kwamba ufahamu huleta hamasa ya kuchukua hatua kuelekea katika mabadiliko.

Ili kujenga ufahamu, Hakikazi ilisambaza taarifa za Sera kwa lugha rahisi kuhusu nyaraka za mfumo wa sera kama vile Mkakati wa Kuondoa Umaskini na sera za sekta maalum kama vile misitu, kilimo na ufugaji nyuki.

Elimu ya sera ilikuwa kama chachu ya utayarishaji wa mipango ya utekelezaji. Zana shirikishi zilitumika kusaidia mchakato.

Mipango ya utekelezaji iliyoanzishwa na jamii ya Karangai, mwanzoni ilikuwa ni:.

Mada mbalimbali mahsusi kwa makundi madogo kwa mfano vitalu vya miti, kilimo cha mboga, ufugaji wa mbuzi na utengenezaji matofali. Aina ya pili ilikuwa Mpango wa Utekelezaji wa Kijiji uliolenga masuala ya maendeleo ya kijamii kama upanuzi wa shule.

Mipango ilitumika kama zana za uraghbishi katika njia kuu tatu. Kwanza, mipango ya utekelezaji wa kijiji iliingizwa kwa kufuata ngazi za mfumo msonge wa kawaida wa utawala wa serikali za mitaa kwa kuziwasilisha kwa kamati ya maendeleo ya kata na kutoka hapo zikaenda kwenye ngazi ya Mipango ya Wilaya.

Hata hivyo kwa upande mwingine mipango ilipelekwa upesi wilayani kwa ajili ya kushawishi huduma na ushauri unaopatikana katika ngazi hizo na fursa kama vile za PADEP.

Tatu, Mipango ya Sekta Mahsusi ilibadilika kwa kuboresha katika muundo wa maendeleo ya jamii na uboreshaji wa hali ya maisha.

Makundi ya ustawi wa hali ya maisha yameanzishwa kwa wafugaji wote wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa. Kikundi cha wafugaji wa mbuzi kimeacha ufugaji holela wa mbuzi kwa ajili ya kupunguza uharibifu wa mazingira. Makundi mengine wanalima kilimo cha mahindi, wanapanda miti, na kulima mboga.

Wenyeji sasa wanahisi kwamba wamejengewa uwezo wa kumiliki mchakato wa maendeleo yao. Muhimu zaidi, wanajihisi kwamba mustakabali wao wa kimaisha unayo matumaini na kwamba wanaangalia mbele kwa matumaini.



"mradi wa ufugaji wa mbuzi umeimarisha afya ya wajukuu zangu. Sasa naweza kukamua lita tatu za maziwa jioni kwa mbuzi mmoja, ambayo tunayatumia kwa mahitaji ya familia na mengine tunayauza kwa kujiongezea kipato. Kutoka kwenye mauzo ya maziwa na vitoto vya mbuzi nimeweza kujenga nyumba ya matofali na kuiezeka mabati"

Mama Ndemanyiso Elirehema- Kijiji cha Karangai

# HABARI KWA LUGHA RAHISI

Wahariri wa mwongozo kwa lugha nyepesi wa Hakikazi wamekuwa na kazi nyingi kipindi hiki. Miongozo ya mkakati wa maendeleo ya sekta ya Kilimo, na Tathmini shirikishi ya Umasikini Tanzania ndio zimechapishwa hivi karibuni.

Majarida mengine mengi bado yanaendelea kuandaliwa. Haya yanajumuisha miongozo ya Mkakati wa Taifa wa Kukuza na Kuondoa Umasikini (MKUKUTA), taarifa ya Maendeleo ya Watu na Umasikini, Sheria na Sera ya Maendeleo ya Ushirika, jarida linalojumuisha Sera ya Taifa ya biashara na Sera ya viwanda vidogo na kati na mwisho ni jozi tatu ya majarida kwa ajili ya kutumika kama sehemu ya programu inayokusudia kuimarisha uwezo wa uraghbishi wa asasi za wafugaji, (angalia makala ya ukurasa uliotangulia).

Kuelekea mwishoni mwa mwaka 2004, Hakikazi ilikamilisha muhtasari wa Sera na Sheria za Ardhi na Maliasili ambayo iliangalia sheria na sera katika maeneo ya misitu, wanyama pori na ardhi.

Majarida mahsusi yalitolewa kuhusu sera zinazohusiana na ufugaji nyuki na misitu. Majarida haya matatu ya mwisho, kwa Pamoja Sera maendeleo ya ushirika na Sera ya biashara zimeshika nafasi kubwa katika utekelezaji wa programu ya utetezi ya Hakikazi, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo wazalishaji na wafanyabiashara wadogo kushawishi sera kwa manufaa na kwa matumizi ya fursa zinazotokana na Sera hizo katika kufanikisha hali ya maisha endelevu.

# MAONI YA MKURUGENZI

Mkakati wa Kukuza na Kuondoa Umasikini wa Taifa (MKUKUTA) uliochapishwa hivi karibuni, unagusa sera zote za serikali kwa miaka mingi ijayo. Kwa hali hiyo, inawakilisha fursa mpya kwa jumuiya za kijamii za Kitanzania kufanya uhamasishaji kwa maslahi ya walio masikini.

Jumuiya za kijamii zinapaswa ziamini kuwa, kuna utashi halisi wa kisiasa katika kutekeleza vipengele vya mkakati na kwamba njia ya kusonga mbele ni kuhakikisha kwa vitendo, kwamba utashi huo umetafsiriwa katika matokeo madhubuti.

Kwa hatua hii, inafaa kusema kwamba jumuiya nyingi za kijamii zimeuchambua MKUKUTA na utekelezaji wake kwa ajili ya kubainisha hatua zilizopendekezwa kuchukuliwa haraka kwa manufaa ya waliowekwa pembeni katika jamii yetu. Kutakuwepo pia na fursa ya kuthibitisha kutambua mikingano baina ya Mkakati, sera zilizopo na sheria.

Upana wa waraka na majukumu yake kama mhimili wa sera zingine unamaanisha kuwa hakuna mapungufu katika vipengele vitakavyoweza kuwa na muelekeo na ufuatiliaji wenye kuleta mafanikio.
Kuna hatua zinazokusudia kukuza sekta za viwanda vidogo na vya kati, kuimarisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo, kurekebisha sheria za ardhi na kutangaza mgawanyo wa bajeti kwenye mbao za matangazo hadi ngazi ya kijiji – n.k.

Changamoto kwa jumuiya za kijamii ni kuhakikisha kwamba watu wanaelewa na kuchambua vipengele vya mkakati kwa njia ambayo itawawezesha kutambua njia za kujihusisha kwenye mchakato.
Kusudi la msingi litalenga kushawishi mabadiliko yatakayoleta umiliki wa mkakati kwa wale ambao wanaohitaji kutumia hatua zilizomo ndani ya mkakati wa kuondokana na umasikini.

Mojawapo ya mahitaji muhimu ya awali kwa mafanikio ya maendeleo ya jamii ni mshikamano wa dhati wa jamii inayohusika.

Jumuia lazima ziingie kwenye mchakato wa kujenga ufahamu na mazungumzo kuhusu sera zao za mazingira kama kundi moja linaloshikamana. Hii itaongeza uwezo uliopo wa kuchambua na kubainisha fursa. Mabadiliko yatakapotokea, yatanufaisha idadi kubwa ya watu.

Cha muhimu, asasi imara na shirikishi ndani ya jamii pia zitaongeza uwezo wa kuhimiza uwajibikaji kwa upande wa serikali kutochukua hatua na utendaji.

Kwa zaidi ya miezi kadhaa ijayo, Hakikazi itafanyakazi na makundi ya wafanyabiashara wadogo na wazalishaji wadogo ambao wanategemea maliasili na mazingira kwa nia ya kujenga uwezo wao wa kuchambua zile sera ambazo zinahusiana zaidi na hali zao. Sera na sheria hizi ni pamoja na zile zinazoendana na ardhi, misitu, kilimo, ushirika na maendeleo, viwanda vidogo na vya kati, biashara na MKUKUTA.

Utendaji katika eneo letu la kazi la Kaskazini mwa Tanzania, programu yake itajumuisha utafiti shirikishi kujifunza namna serikali kuu na serikali za mtaa zinavyowajibika katika maeneo ya kilimo na masoko.

Kujenga uwezo wa hali ya maisha ya jamii pia utatiliwa mkazo, kwa kufikisha ngazi ya Taifa taarifa zitokazo kwenye jamii kwa sera zilizopo. Programu ilipangwa kuendelea hadi mwishoni mwa mwaka 2006, lakini kusudio letu litakuwa kudumisha uhusiano wa kikazi wa muda mrefu na jamii tunazozilenga.



Emmanuel Kallonga,
Mkurugenzi, Hakikazi Catalyst.

